

**HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA ELIMU YA JUU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA,
MHESHIMIWA PROF. PETER M. MSOLLA (MB), WAKATI WA KUWASILISHA
BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2007/2008**

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii inayohusu Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2007/2008.
2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote, sina budi kuwapongeza Waheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro kwa kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Dkt. Batilda Salha Burian (Mb) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu-Bunge, Benard Membe (Mb) kuwa Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Gaudence Cassian Kayombo (Mb) kuwa Naibu Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na William Mganga Ngeleja (Mb) kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Vile vile niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliojiunga na Bunge hili kwa kuchaguliwa na kuteuliwa, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru na Mheshimiwa Florence Essa Kyendesha, Mbunge wa viti Maalum. Naomba pia niwapongeze waliochaguliwa kuwakilisha nchi yetu ya Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki, ambao ni Mheshimiwa Dkt. Didas John Massaburi, Mheshimiwa Dkt Aman Walid Kabourou, Mheshimiwa Dkt. George Francis Nangale, Mheshimiwa Sylvia Kate Kamba na Mheshimiwa Septuu Nassoro, Mheshimiwa Dkt. Said Gharib Bilal, Mheshimiwa Dkt Janet Deo Mmari na Mheshimiwa Dkt. Fortunatus Lwanyatika Masha.
3. **Mheshimiwa Spika**, aidha napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge, ndugu jamaa na marafiki katika kuwafaraji na kuwapa pole familia, ndugu, na wapiga kura wa marehemu **Mheshimiwa Juma Jamaldini Akukweti** aliyekuwa Waziri

- wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge), Mbunge wa Tunduru na **Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia**, Mbunge wa viti maalumu (CCM). Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.
4. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioweza kutekeleza majukumu ya Wizara yangu kwa kipindi kilichopita, na ambao wamewezesha kuandaa mipango ya mwaka 2007/2008 na kuboresha hoja yangu ambayo naiwasilisha katika hotuba hii. Aidha, natoa shukrani kwa wananchi wote wa Tanzania kwa mchango wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu. Natoa shukrani zangu za pekee kwa **Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Gaudentia Mugosi Kabaka (Mb); Katibu Mkuu Dkt. Naomi Bakunzi Katunzi**, Watendaji katika Wizara yangu pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara, mashirika mbalimbali ya ndani na nje kwa misaada na ushauri wao. Kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii chini ya Mwenyekiti wake **Mheshimiwa Omar Kwaang'w** Mbunge wa Babati Mjini (CCM) kwa ushauri wao. Aidha, napenda kumshukuru **Mheshimiwa Suzan Anselm Jerome Lyimo** Mbunge wa viti maalum (CHADEMA) ambaye ni msemaji mkuu wa kambi ya upinzani kuhusu Wizara yangu na Waziri Kivuli kwa ushirikiano wake na mchango wake katika kuiboresha hoja hii.
5. **Mheshimiwa Spika**, Wizara katika kipindi cha kuanzia Julai, 2006 imeendelea na utekelezaji wa majukumu na mipango yake kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 - 2010, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini, Sera ya Elimu ya Juu, Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo, Sera ya Sayansi na Teknolojia, Mpango Kabambe wa Wizara, pamoja na ahadi na maagizo mbalimbali ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipoitembelea Wizara tarehe 1 Februari, 2006. Hivyo lengo la taarifa hii ni kueleza hali ya utekelezaji wa ahadi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2006/2007 na malengo ya wizara pamoja na makisio ya bajeti kwa mwaka 2007/08.

MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2006/2007

6. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/07 wizara yangu kupitia Idara na Taasisi zake imefanikiwa kutekeleza ahadi nyingi ilizozitoa Bungeni mwaka jana. Naomba niwasilishe utekelezaji na mafanikio kama ifuatavyo:-

IDARA YA ELIMU YA JUU

7. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/07 Idara ya Elimu ya Juu imetekeleza yafuatayo:

Imeongeza idadi ya wanafunzi katika Elimu ya Juu kutoka wanafunzi 52,108 hadi 68,029 ambalo ni ongezeko la asilimia 30.6 ukilinganisha na udahili wa mwaka 2005/06.

Imehakikisha mitaala ya elimu ya juu inakidhi mahitaji ya soko la ajira na kujiajiri.

- Imedhamini wanafunzi 1,422 wa shahada ya kwanza ya Udaktari (MD) katika vyuo vikuu nchini.

Imedhamini wanafunzi 90 raia wa Uganda, ikiwa ni utekelezaji wa mkataba wa kubadilishana wanafunzi wa shahada ya kwanza katika Vyuo vikuu vya Afrika ya Mashariki.

Imeendelea na udhamini wa mafunzo ya wanafunzi watano, raia wa China ikiwa ni utekelezaji wa mkataba wa ushirikiano kati ya Tanzania na China.

Imeelimisha umma kuhusu Sera ya uchangiaji wa elimu ya juu.

Imepitia rasimu ya Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999 iliyohuishwa na ambayo imejadiliwa na wadau mwezi Juni, 2007.

Imekamilisha mchakato wa kuwapata viongozi wa vyuo vikuu vya Ardhi na Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili.

Imeendelea na udhamini wa mafunzo ya wanataaluma themanini (80) katika vyuo vikuu vya umma.

IDARA YA ELIMU YA UFUNDI

8. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Idara ya Elimu ya Ufundi ilitekeleza yafuatayo:-

Ilidhamini mafunzo kwa wanafunzi 1,754 katika ngazi ya Ufundi Sanifu katika Vyuo na Taasisi za Ufundi zilizo chini ya Wizara.

Iligharimia mafunzo ya watumishi kumi na wawili (12) wa Chuo cha Ufundi Arusha na Makao Makuu katika ngazi ya udaktari wa falsafa (4) na Shahada ya Uzamili (8).

Iiratibu na kugharamia mafunzo maalumu ya ualimu (Pedagogical Skills) kwa wahandisi 23 walioajiriwa katika Chuo cha Ufundi Arusha.

IDARA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

9. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Idara ya Sayansi na Teknolojia ilitekeleza yafuatayo:

- Iliandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Utafiti na kujadiliwa na Sekretariati ya Baraza la Mawaziri.
- Iliendeleza mchakato wa urejaji wa Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia kwa madhumuni ya kutunga Sera mpya ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.
- Iliendeleza taratibu za uanzishwaji wa Taasisi ya Nelson Mandela, katika eneo la kudumu lililoko Karangai katika Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru, Arusha.

- Iliendelea kuelimisha jamii kupitia vipindi 52 vya Radio na maonyesho kuhusu elimu ya juu, Sayansi na Teknolojia.
- Iitoa jumla ya tuzo 119 kwa wanafunzi wa kike kutoka shule 20 zilizofanya vizuri katika masomo ya Sayansi na Hisabati katika mitihani ya kumaliza kidato cha nne mwaka 2006 (18); kidato cha sita mwaka 2006 na 2007 (25); vyuo vikuu, taasisi za serikali na binafsi za Elimu ya Juu na Ufundi (43). Aidha wizara pia ilitoa tuzo 33 kwa shule za sekondari zilizowezesha wanafunzi hao kufanya vizuri katika masomo hayo.

IDARA YA SERA NA MIPANGO:

10. Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa fedha 2006/2007 Idara ya Sera na Mipango ilitekeleza yafuatayo:

- Iliratibu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005-2010, na kuandaa taarifa ya utekelezaji.
- Iliratibu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo 21, katika Taasisi na Makao Makuu. Kati ya miradi hiyo, 18 ni miradi inayogharamiwa na fedha za ndani na 3 inagharamiwa na fedha za nje.
- Iliratibu uanzishwaji wa Chuo Kikuu cha Dodoma, ambapo upembuzi yakinifu umekamilika na kujadiliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, Kamati ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri.
- Iliratibu shughuli za ushirikiano wa Kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuhudhuria Vikao vya EAC, SADC na kuingia Mikataba ya Maridhiano (MOU) na nchi marafiki.
- Iliratibu maandalizi ya mpango maalum (Quickwin Programme) kwa ajili ya kuendeleza Elimu ya Juu na Ufundi utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

- Iiratibu maandalizi ya mkakati wa kuendeleza Elimu Juu na Ufundi (Higher and Technical Education Development Programme) ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi linalotokana na mafanikio ya Mpango wa Elimu ya Msingi (MEM) na Sekondari (MES).

IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI

11. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Idara ya Utawala na Utumishi ilitekeleza yafuatayo:-

- Iiratibu mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa watumishi arobaini na saba (47) ili kuwaongezea ujuzi maarifa na ufanisi katika utendaji wao kazi.
- Iiendelea kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma zisizo rasmi (non-core services) Makao Makuu pamoja na Chuo cha Ufundi Arusha, hususani huduma za ulinzi, usafi na chakula.

Iiratibu upatikanaji wa vibali vya ajira 1,528 katika vyuo vikuu na Taasisi zake kwa lengo la kupunguza uhaba wa wafanyakazi.

Iliadhimisha siku ya UKIMWI ya Wizara kwa kufanya shughuli mbalimbali zinazohusu upimaji UKIMWI kwa hiari, matumizi ya dawa za kurefusha maisha kwa waishio na virusi vya UKIMWI na kupunguza maambukizo ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Pia iliandaa mwongozo wa kushughulikia taratibu za kutoa lishe na matibabu kwa watumishi waishio na virusi ya UKIMWI.

Ilijiri watumishi kumi na nne (14) kati ya hao wawili (2) Makao Makuu na kumi na mbili (12) Chuo cha Ufundi Arusha. Aidha, watumishi 22 wamepandishwa vyeo na 3 kuthibitishwa kazini.

VYUO VIKUU:

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (KAMPASI YA MLIMANI)

12. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Kampasi ya mlimani) kilitekeleza yafuatayo:

- Kilidahili jumla ya wanafunzi 6,027, kati yao wanafunzi wa Shahada ya kwanza ni 3,890 wanafunzi wa kike ni 1,400 sawa na 36% na Shahada ya Uzamili ni 2,137 wanafunzi wa kike ni 577 sawa na 27%.
- Kiliendeleza juhudi za kutumia teknolojia ya mawasiliano (ICT) katika kufundisha na kujifunza kwa kutumia Kituo cha Elimu Endelevu (Centre for Continuing Education), kuwafundisha wahadhiri mbinu mpya na bora za kufundishia pamoja na kuimarisha mtandao wa ndani (Local Area Network)
- Kiliajiri watumishi 281 wanataaluma 185 na waendeshaji 96 katika ngazi mbalimbali kwenye idara 17 zenye upungufu mkubwa wa wafanyakazi.
- Kiliendelea kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi kugharamia utafiti kulingana na sera ya utafiti ya chuo.
- Kiliendelea kutumia mikakati mbalimbali pamoja na kutoa mafunzo maalum kwa wasichana wanaotaka kujiunga na programu za sayansi, uhandisi na teknolojia, uchumi na takwimu, ili kuinua uwiano wa wavulana kwa wasichana.
- Kiliendeleza ujenzi wa madarasa mawili yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 1,000 kila moja kwa wakati mmoja. Ujenzi umefikia asilimia 70.

- Kilikamilisha ujenzi wa msingi wa jengo la Utawala la Taasisi ya Sayansi za Bahari iliyopo Buyu Zanzibar.
- Kilikamilisha ujenzi wa kitengo kitakachotumiwa na kituo cha ujasiriamali.
- Kilikamilisha ujenzi wa awamu ya kwanza ya mradi wa Mlimani City.
- Kilikabidhiwa majengo yaliyokuwa ya Kampuni ya Simu Tanzania (TTCL) yaliyoko Kijitonyama, kwa ajili ya Kitivo cha Uhandisi Umeme na Mifumo ya Kompyuta cha Kampasi ya Uhandisi (COET).
- Kiliendelea na ukarabati wa Mabweni ya wanafunzi husasan bweni Na. 2 na Na. 5.

CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

13. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilitekeleza yafuatayo:

- Kilidahili jumla ya wanafunzi 1,089 kati ya hao Shahada ya kwanza ni wanafunzi 820 wanafunzi wa kike wakiwa ni 33% na Shahada Uzamili 269 wanafunzi wa kike wakiwa 30%.

Kiliimarisha tafiti zinazolenga kuboresha kilimo, mifugo na maliasili mfano kilimo cha mboga na matunda katika vijiji vya Mvomero, Mgeta, Mkuyuni, Kiroka, Matombo na Bunduki mkoani Morogoro.

- Kilianzisha majaribio ya kutumia panya buku kutambua kuwepo kwa vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu (TB) pamoja na panya hao kuendelea kutumika katika kufichua mabomu. Matokeo ya awali yameonyesha kwamba panya buku wana uwezo mkubwa wa kutambua TB kwa kunusa makohozi ya wagonjwa kwa kasi zaidi kuliko binadamu anapotumia darubini.

- Kilifanya warsha/kongamano (19) za kisayansi ambazo ziliwashirikisha wanataaluma na wadau ndani na nje ya nchi.
- Kiliendesha kozi fupi, semina na kutoa huduma za ushauri wa kilimo, utunzaji na usimamizi wa mali ya asili, misitu, na ufugaji kwa wakulima na wafanyakazi.
- Kilikamilisha ujenzi wa maktaba iliyopo Kampasi ya Solomon Mahlangu na jengo la Ujasiriamali na Biashara.
- Kilikarabati madarasa 3, mabweni 12, maabara 1 na nyumba za wafanyakazi 4.

CHUO KIKUU MZUMBE

14. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Mzumbe kilitekeleza yafuatayo:

- Kilidahili wanafunzi 816 wa Shahada ya kwanza, kati ya hao wanafunzi wa kike ni 358 sawa na 44% na wa kiume ni 458. Aidha Chuo kilidahili wanafunzi 282 wa Shahada ya Uzamili kati yao wanafunzi 133 ni wa kike sawa na 47%.
- Kiliendelea na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 300 katika kampasi ya Mbeya. Ujenzi huu utakamilika mwezi Septemba, 2007.
- Kilisomesha Wahadhiri watano (5) shahada ya uzamili na tisa (9) masomo ya Shahada ya Uzamivu.
- Kilikamilisha tafiti ishirini na moja (21) katika maeneo ya Sayansi ya Jamii, maeneo hayo ni;
 - "Public Private Partnership"
 - "Environment"
 - "HIV/AIDS"
 - "Financial Management"
 - "Administration"

- Kilinunua kompyuta 130 kwa ajili ya kuboresha ufundishaji.
- Kilikamilisha upanuzi wa maktaba ya Chuo, kampasi ya Mzumbe.
- Kiliendelea na ujenzi wa mabweni ya wanafunzi na ofisi

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

15. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kilitekeleza yafuatayo:

- Kilidahili wanafunzi 3,868 kati ya hao Shahada ya kwanza ni wanafunzi 3,354 wanafunzi wa kike wakiwa 987 sawa na 29% na Shahada ya uzamili 514 kati ya hao wanafunzi wa kike wakiwa 58 sawa na 11%.
- Kilikarabati ofisi za wafanyakazi makao makuu na katika mikoa ya Iringa, Dodoma na kuzindua rasmi majengo ya mkoa wa Singida.
- Kiliongeza idadi ya wanataaluma na waendeshaji ili kuimarisha utendaji. Idadi ya wanataaluma imefikia 181, waendeshaji 166 na mafundi wa TEKNOHAMA 10.
- Kilianzisha vituo vipya katika wilaya tatu (3) za mkoa wa Dar es salaam, ili kukabiliana na idadi kubwa ya wanafunzi.
- Kiliimarisha huduma za maktaba kwa kuongeza majengo na muda wa matumizi katika mkoa wa Dar es salaam.

CHUO KIKUU CHA DODOMA (THE UNIVERSITY OF DODOMA)

16. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/07 nilitoa taarifa kuhusu nia ya Serikali ya kuanzisha Chuo Kikuu kipya hapa Dodoma. Napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Serikali imeanzisha Chuo Kikuu hicho kinachoitwa Chuo Kikuu cha Dodoma (The University of Dodoma).

Chuo hiki kipo katika eneo la Chimwaga ambapo jumla ya hekta 6,000 zimetolewa na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) kwa ajili ya ujenzi wa chuo. Kwa sasa chuo kinaendesha shughuli zake katika jengo la Chimwaga. Katika miezi takribani 7 ya uhai wake, Chuo Kikuu cha Dodoma kimeweza kutekeleza yafuatayo:

- Kimerekebisha jengo la Chimwaga (Remodeling), ili kupata vyumba 31 kati ya hivyo vyumba 15 ni ofisi na 16 ni madarasa. Kati ya madarasa hayo 3 yana uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 360, madarasa 5 yana uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 na madarasa 8 yana uwezo wa kuchukua wanafunzi 360.
- Kimenunua samani kwa ajili ya ofisi, vyumba vya mihadhara na kwa ajili ya malazi ya wanafunzi.
- Kimekarabati nyumba moja itakayotumika kama Zahanati.
- Kimepata watendaji wakuu wakiwemo; Mkuu wa Chuo, Mwenyekiti wa Baraza, Makamu Mkuu wa Chuo na Makamu Wakuu wa Chuo wawili.
- Kimetangaza nafasi za kazi kwa ajili ya wanataaluma 80 na waendeshaji 134.
- Kimetangaza nafasi za masomo katika fani za Elimu, Sayansi ya Jamii na Sayansi za Kompyuta.

VYUO VIKUU VISHIRIKI

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA SAYANSI ZA AFYA MUHIMBILI

17. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili kilitokeleza yafuatayo:

- Kilidahili jumla ya wanafunzi 331 kati ya hao wanafunzi wa kiume ni 230 na wa kike ni 101 sawa na 31%.

- Kilikamilisha maandalizi ya kukifanya Chuo Kikuu kamili cha Tiba na Sayansi za Afya (Muhimbili University of Health and Allied Sciences-MUHAS)
- Kilikamilisha ukarabati wa Mabweni ya wanafunzi yaliyopo barabara ya Chole Dar es salaam.
- Kiliendelea na ujenzi wa kumbi mbili (2) za kufundishia zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 350 kila moja kwa wakati mmoja na vyumba 40 vya ofisi.
- Kiliendelea na uendelezaji wa miundombinu ya Chuo huko Mloganzila Mkoa wa Pwani kwa kushirikiana na TANROADS
- Kiliendelea na utafiti wa magonjwa ya binadamu hususan UKIMWI (chanjo), Kifua kikuu, Malaria na magonjwa ya wanawake.
- Kilikamilisha upanuzi wa maktaba ya Chuo.

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ARDHI NA USANIFU MAJENGO

18. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo kilitokeleza yafuatayo:

- Kilidahili wanafunzi 466 wa shahada ya kwanza kati ya hao 375 ni wa kiume na 91 ni wa kike sawa na 20% .
- Kilikamilisha maandalizi ya kukifanya kuwa Chuo Kikuu kamili cha Ardhi (Ardhi University).
- Kilitayarisha mitaala itakayoweza uanzishwaji wa idara mpya 16 badala ya 6 za sasa, na hivyo kufanya idadi kuwa 22.

Kiliimarisha matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika ufundishaji kwa kununua kompyuta sitini (60).

- Kiliajiri wahadhiri na watafiti ishirini na saba (27) na wafanyakazi waendeshaji kumi na moja (11).
- Kilikamilisha ukarabati wa awali wa baadhi ya mabweni, ofisi, madarasa na nyumba za wafanyakazi.
- Kilikamilisha ukarabati wa jengo la zamani la utawala kuwa maktaba na madarasa.

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU CHA DAR ES SALAAM

19. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam kilitekeleza yafuatayo:

Kilidahili wanafunzi 1,479 kati ya hao wa kiume ni 833 na wa kike 646, sawa na 44%.

Kiliajiri walimu 103 kati yao 3 wana Shahada ya Udaktari wa Falsafa, 39 Shahada ya Uzamili na 61 Shahada ya kwanza. Pia Chuo kiliajiri wafanyakazi waendeshaji 191 kati yao 66 ni walimu wa Shule za Awali, Msingi na Sekondari, shule hizo zinamilikiwa na kuendeshwa kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa walimu wanafunzi.

- Kilipanua maktaba na kununua vitabu 316 vya kufundishia na kujifunzia.

Kilinunua vifaa vya maabara.

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA USHIRIKA NA STADI ZA BIASHARA MOSHI

20. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara – Moshi kilitokeleza yafuatayo:

- Kilidahili wanafunzi 403 kati ya hao 69 ni kwa ajili ya Diploma ya Uzamili na 334 ni kwa ajili ya Shahada ya kwanza.
- Kiliimarisha mtandao wa kompyuta kwenye maktaba.
- Kiliendeleza mafunzo ya wafanyakazi wanataaluma kumi (10) kufikia kiwango cha Udaktari wa Falsafa.
- Kiliboresha shughuli za utafiti na uchapishaji.
- Kiliendelea kuboresha kiwango cha huduma za uelekezi na ushauri.

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU CHA MKWAWA

21. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Mkwawa kilitokeleza yafuatayo:

Kilidahili wanafunzi 917 kati ya hao, wanafunzi wa kiume ni 656 na wa kike 301 sawa na 33%.

Kiliendelea na ukarabati wa mabweni, madarasa na kuweka samani.

Kilikarabati na kupanua jengo la maktaba.

- Kiliendelea na ukarabati wa zahanati.
- Kilikarabati barabara, miundombinu ya maji safi na maji taka.

Kiliweka samani katika mabweni ya wanafunzi yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 889.

Kilitoa mafunzo maalum kwa wanafunzi wa kike katika masomo ya Sayansi ili kuinua uwiano wa wanafunzi wa kike kwa wa kiume.

- Kiliajiri wafanyakazi waendeshaji 65 na wahadhiri 56

TAASISI

TAASISI YA UANDISHI WA HABARI NA MAWASILIANO YA UMMA

22. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma ilitekeleza yafuatayo:

- Ilidahili wanafunzi 301, kati ya hao wavulana ni 187 na wasichana 114, sawa na 38%.
- Ilongeza madarasa mawili yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi sitini (60) kila darasa.
- Iliendesha kituo cha Radio – Radio Mlimani FM kwa kutoa ushauri wa kitaalam katika masuala ya habari, mawasiliano ya umma, matangazo na utangazaji.

TAASISI YA TEKNOLOJIA DAR ES SALAAM

23. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilitekeleza yafuatayo:

- Ilidahili jumla ya wanafunzi 793 wa mwaka wa kwanza katika programu za Shahada ya Uhandisi 278, Stashahada ya Ufundi sanifu 411 na Cheti cha Ufundi sanifu 104. Aidha, kati ya wanafunzi 411 wa stashahada ya Ufundi Sanifu waliodahiliwa, 23 ni wa fani ya Uhandisi Migodi.

- Ilikamilisha mtaala wa programu ya mafunzo ya Shahada ya Uzamili ya Ukarabati (Culture of Maintenance).
- Iligharimia mafunzo ya wafanyakazi 16 wa Taasisi katika masomo ya muda mrefu na 5 katika masomo ya muda mfupi.
- Iliendesha mafunzo maalum kwa wanafunzi wa kike na kufanikiwa kudahili 23 baada ya kupata sifa za kujiunga na Taasisi.
- Ilikamilisha utafiti wa udongo sehemu ya ujenzi (soil testing), maombi ya kibali cha ujenzi, michoro ya ujenzi (structural drawings) na taratibu za kumpata Msimamizi wa Ujenzi (Consultant), kwa ajili ya kuanza ujenzi wa "Teaching Tower" ili kuongeza madarasa, maabara na ofisi za wafanyakazi.

TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA

24. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya ilitekeleza yafuatayo:

- Ilidahili wanafunzi 175 wa mwaka wa kwanza katika ngazi ya Ufundi Sanifu kati yao 18 ni wasichana sawa na 10% na 34 wa Stashahada ya Juu ya Uhandisi.
- Iligharamia mafunzo ya walimu 10. Kati ya hao 5 wanachukua mafunzo ya uzamili, 3 mafunzo ya udaktari wa falsafa na 2 wanasoma Shahada ya kwanza. Aidha, wafanyakazi 4 wasiokuwa walimu wanasomea mafunzo mbalimbali hapa nchini.

Ilijiri wafanyakazi 146 wanataaluma ni 76 na waendeshaji 70.

- Ilikamilisha ukarabati wa bweni moja lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 300.

VYUO:

CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE

25. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kilitekeleza yafuatayo:

- Kilidahili wanafunzi 53 wa Shahada ya Kwanza ya Siasa na Uendeshaji wa Maendeleo ya Jamii, ikiwa na wanaume 32 na wanawake 21 sawa na 40%. Aidha, kilidahili wanafunzi 50 wa Shahada ya Kwanza ya Uchumi kuhusu Maendeleo, ikiwa na wanaume 36 na wanawake 14 sawa na 28%.

Kiliajiri wanataaluma 22 wanaume 12 na wanawake 10 sawa na 45% na wafanyakazi waendeshaji 20 kati yao wanaume 11 na wanawake 9 sawa na 45%. Ajira hizo zilikiwezesha Chuo kuanza kuendesha mafunzo ya Shahada ya Kwanza.

- Kilikamilisha Mpango Mkakati wa Chuo wa miaka kumi, 2007 – 2016.
- Kiligharamia mafunzo ya watumishi watatu, kati ya hao mmoja Shahada ya Uzamili, mmoja Shahada ya Kwanza na mmoja Stashahada ya Juu.

CHUO CHA UFUNDI ARUSHA

26. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Chuo cha Ufundi Arusha kilitekeleza yafuatayo:

- Kilidahili wanafunzi 134 wa ngazi ya ufundi Sanifu kati ya hao wavulana ni 120 na wasichana 14 sawa na 10%.

- Kiliendesha mafunzo na semina juu ya kujikinga na UKIMWI kwa walimu, wafanyakazi na wanafunzi.
- Kilikamilisha ukarabati wa Hosteli ya wasichana yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 200.
- Kilichimba kisima cha maji safi (Bore hole) chenye uwezo wa kutoa lita 8,000 kwa saa.

TUME

TUME YA TAIFA YA UNESCO

27. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 Tume ya Taifa ya UNESCO ilitekeleza yafuatayo:

- Ilisimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi, pamoja na kufanya tathmini ya miradi inayoendelea na ile iliyoidhinishwa na UNESCO kwa kipindi cha 2006/2007 kama ilivyoamuliwa katika Kikao cha 33 cha Mkutano Mkuu wa UNESCO.
- Iliandaa kongamano kuhusu Mwaka wa Kimataifa wa Sayari Dunia lililofanyika Da es Salaam, mwaka 2006. Kamati ya Kitaifa imeundwa na inaandaa Mkutano wa Kanda ya Afrika utakaofanyika mwezi Mei, 2008 mjini Arusha.
- Iliandaa rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri (WBLM) kuhusu Tume ya UNESCO kuwa chombo kinachojitegemea na kupitishwa na Baraza la Mawaziri. Muswada wa Sheria unakamilishwa.
- Imeratibu ukamilishwaji wa mchanganuo wa kutafuta fedha za mradi wa Utamaduni wa Ukarabati (Culture of Maintenance). Mchanganuo huo umewasilishwa UNESCO, kwa kuombewa fedha.

- Iliendelea kuratibu mradi unaolenga kuimarisha mafunzo ya Ualimu nchini. Hadi sasa, walimu 36 toka Tanzania Bara na 30 toka Zanzibar wamekwishapata mafunzo ya muda mfupi. Wakufunzi 32 Tanzania Bara na 35 Tanzania Zanzibar wamepata mafunzo ya wiki mbili kuanzia Agosti 2006.
- Ilifuatilia ombi la kuanzishwa Kiti cha UNESCO cha Historia lililoandaliwa na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA). Ombi hili limewasilishwa UNESCO Paris.

TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA

28. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Tume ya Vyuo Vikuu ilitekeleza yafuatayo:

Iliiratibu na kusimamia usajili na upatikanaji wa Hati Idhini 'Charter' kwa vyuo vikuu vya umma vitano (5) na vyuo vikuu vishiriki vitano (5). Hati hizi zimesainiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na zimeanza kutumika katika Vyuo husika.

Iliendelea kuboresha taratibu za udahili.

- Iliandaa na kuratibu maonyesho ya pili ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia mwezi Agosti, 2006.
- Iliendelea kutoa machapisho ya kuelimisha umma na kuhamasisha wawekezaji kuanzisha vyuo vikuu bora.
- Iliendeleza ushirikiano na mabaraza ya Ithibati ya Elimu ya Juu duniani.
- Ilitathmini na kutoa Hati za Usajili wa muda wa Vyuo Vikuu vinne (4) ambavyo ni:-

Chuo Kikuu Kishiriki cha Sebastian Kolowa - Lushoto

Chuo Kikuu cha Mtakatifu John – Dodoma

Chuo Kikuu Kishiriki cha Kumbukumbu ya Stefano - Moshi

Chuo Kikuu cha Dodoma.

- Ilikagua kwa lengo la kusajili upya Vyuo Vikuu vitano (5) na Vyuo Vikuu Vishiriki vitano (5) vinavyomilikiwa na Serikali ambavyo ni:-

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo.

Chuo Kikuu Mzumbe

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Chuo Kikuu cha Serikali cha Zanzibar

Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Muhimbili

Chuo Kikuu Kishiriki cha Ardhi na Usanifu Majengo

Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara cha Moshi

Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Dar es Salaam

Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu cha Mkwawa.

Iliendelea kusimamia na kupitisha udahili wa wanafunzi wanaojiunga na Vyuo Vikuu nchini.

Ilitathmini vyeti 188 kwa lengo la kuvichambua hadhi na uhalali wake. Kati ya vyeti hivyo vilivyokubalika ni 174 vilivyoshushwa daraja ni 6 na ambavyo havikutambuliwa ni 8.

TUME YA TAIFA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

29. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Tume ilitekeleza yafuatayo:-

Iliendelea na uhawilishaji wa Teknolojia mbali mbali zilizohakikiwa ikiwa ni pamoja na;

- o Kuwafundisha wakufunzi 60 kutoka mikoa ya Dar es Salaamu, Dodoma, Singida, Shinyanga, Morogoro na Mbeya teknolojia ya kutengeneza majiko sanifu. Wakufunzi hao waliweza kusimamia uzalishaji wa majiko takribani 10,000 katika mikoa yao.

Kuwajengea uwezo wajasiriamali wawili wa Kiwira Coal mine na Space Engineering kuingiza Teknolojia ya matumizi ya makaa ya mawe ya kibaolojia (Coal Biomass Briquettes) katika soko.

Kuwezesha ujenzi wa nyumba za gharama nafuu. Utalaamu huu umetumika katika ujenzi wa nyumba ya pampu ya maji Dar es Salaam na madarasa manne ya shule ya sekondari mkoani Singida.

Ilikamilisha tathmini ya mahitaji ya teknolojia katika mikoa ya Dar es Salaamu, Pwani na Morogoro. Aidha katalogi ya teknolojia mbali mbali zinazotengenezwa na taasisi za hapa nchini iliandaliwa.

Ilitoa elimu ya hatimiliki na hataza kwa taasisi 8. Aidha, kituo cha kutoa elimu juu ya hataza na hatimiliki kilifunguliwa katika majengo ya Tume kwa kushirikiana na BRELA na WIPO.

Iliendelea na mchakato wa kuunda Benki ya Takwimu (Data base) za Utafiti. Zoezi hili linategemewa kukamilika katika mwaka wa fedha, 2007/08.

Iliendelea na ufadhili wa tafiti mbali mbali za kisayansi katika maeneo ya kipaumbele kitaifa. Tafiti 2 mpya zilifadhiliwa na taarifa 3 za tafiti zilizokamilika kutokana na ufadhili wa miaka iliyopita zilipokelewa.

Iliandaa kongamano la pili la Sayansi na Teknolojia mjini Dar es Salaam, ambapo wanasayansi 66 waliwasilisha maada zao mbele ya wanasayansi na wajasiriamali 150.

Iliendelea kuimarisha mtandao wa taasisi za utafiti na maendeleo, kupanua Masijala ya Utafiti Kuimarisha matumizi ya mifumo ya mawasiliano na habari vijijini na kuhamasisha wananchi kutumia Sayansi na Teknoloji katika harakati za maendeleo kama ifuatavyo:

Jumla ya taasisi, asasi na azise 30 za Utafiti na Maendeleo zimeendelea kupata huduma za internet katika mtandao wa Tume
Ilikamilisha uwekaji Masijala ya utafiti ya Tume katika Mtandao (www.research.or.tz).

Iliendelea kutekeleza mradi wa kusambaza teknolojia ya mawasiliano vijijini (Telecentres) katika wilaya za Bunda, Serengeti na Bagamoyo. Mradi wa mawasiliano katika vijijini vya Bunda na Mugumu Wilayani Serengeti ulizinduliwa tarehe 27 Juni, 2007 na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, Tume iliviwezesha vituo 6 vya mawasiliano na habari vijijini kutoa huduma endelevu. Vituo hivyo ni pamoja na Sengerema, Lugoba, Kilosa, Ngara, Wete na Kasulu. Kati ya hivyo, kituo cha Sengerema kimeweza kujitegemea na kitakabidhiwa Serikali ya Kijiji mwaka huu wa fedha.

Iliendelea kuhamasisha matumizi ya Sayansi na Teknolojia kwa kutoa makala 17 na taarifa 31 katika magazeti mbali mbali na vipindi 20 vya luninga.

Iliwezesha maonyesho 3 ya Sayansi na Teknolojia mjini Dar es Salaam kufanyika katika miezi ya April, Mei na Juni, 2007.

TUME YA NGUVU ZA ATOMIKI TANZANIA

30. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007, Tume ilitekeleza yafuatayo:-

- Ilihakikisha usalama wa wafanyakazi wa mionzi 1300 (katika vituo 250 vinavyotoa huduma za X-rays) kwa kuwapatia huduma ya upimaji wa mionzi (Personnel Radiation Monitoring) na ushauri wa kinga ya mionzi wakiwa kazini.

Ilikagua vituo 171 vya mionzi ayonisha, pamoja na kukagua migodi sita (6) na minara 60 ya simu za mikononi.

Ilipokea maombi 197 kwa ajili ya kupewa leseni ya kutumia vyanzo vya mionzi kutoka vituo vya x-ray, viwandani na katika taasisi za utafiti. Baada ya uchambuzi wa maombi hayo na kutathimini usalama wa vituo husika leseni 170 zilitolewa; na waombaji waliobaki waliagizwa kufanya marekebisho ili kukidhi usalama katika vituo hivyo.

- Iliendelea kudhibiti na kupima vyakula viingizwavyo na kutolewa nchini ili kuhakikisha havikuchafuliwa na viini vya mionzi kwa kiwango kinachoweza kusababisha madhara kwa walaji ambapo sampuli 2,700 zilipimwa.
- Iliendelea kuratibu na kusimamia uingizaji wa teknolojia ya nyuklia, kwa kupitia miradi ya kitaifa na kikanda inayofadhiliwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki.
- Iliratibu utekelezaji wa miradi 8 ya kitaifa na mradi 1 wa kikanda katika maeneo mbali mbali yanayotumia Teknolojia ya nyuklia inayogharimiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomic (IAEA) katika tasisi za hapa nchini.

- Iliendelea kutoa huduma za matengenezo ya vifaa vya elektroniki pamoja na mashine za x-ray ili kuhakikisha matumizi bora na salama ya vifaa hivyo.
- Ilikusanya na kuyahifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi kutoka Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Taasisi ya Utafiti wa Ndorobo Tanga (TPRI), Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Idara ya Fizikia ya Chuo Kikuu Dar es Salaam.
- Ilikamilisha taratibu za matumizi (operational and protocols) wa jengo la kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi Makao Makuu ya Tume Arusha.
- Ilitoa elimu ya kinga ya mionzi kwa wafanyakazi 60 wa vituo vya mionzi ili kuhamasisha na kuhakikisha matumizi salama ya mionzi. Aidha Tume pia iliendelea kuwapatia wataalamu wa Tume mafunzo ya ziada ili kuboresha ufanisi wao wa kazi.
- Iliendelea kuratibu ujenzi na uendeshaji wa Kituo cha kupima mionzi kijulikanacho kama RMS-RN64 kilichojengwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa msaada wa Shirika la Kimataifa Ijulikanalo kwa jina la Comprehensive Nuclear Test Ban Treaty Organization (CTBTO).
- Iliendelea kushirikiana na shirika la Kimataifa la CTBTO katika kudhibiti majaribio ya nguvu za nyuklia kwa ukanda wa Afrika.

MAMLAKA YA ELIMU TANZANIA

31. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Mamlaka ya Elimu Tanzania ilitekeleza yafuatayo:

- Iliendelea kuhamasisha wadau kuchangia na kuwekeza kwenye miradi ya elimu na kupanua wigo wa uchangiaji katika Mfuko wa Elimu kwa kushirikisha wadau katika ngazi ya Wilaya. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2006 hadi Juni, 2007 kiasi cha **Sh 374,000,000** kimechangwa na wadau mbalimbali wa elimu.

- Iliendelea kutoa ruzuku na mikopo kwa vyuo na shule kwa ajili ya miradi mbalimbali ya kuboresha elimu, kuongeza udahili na kuongeza usawa. Kiasi cha Sh.2,364,011,983 na Dola za Kimarekani 68,000 kilitolewa kwa madhumuni hayo.
- Iliendelea kufanya ukaguzi wa miradi iliyofadhiliwa na Mfuko wa Elimu, kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi zilizofaidika na ruzuku na mikopo hiyo.

BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU

32. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2006/2007 Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilitekeleza yafuatayo:

- Iliendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi **51,772** wahitaji wa elimu ya juu wanaostahili katika maeneo yafuatayo:
 - Ada ya masomo
 - Elimu kwa vitendo
 - Mahitaji maalumu ya vitivo
 - Chakula na Malazi
 - Vitabu na viandikio
 - Utafiti.
- Iliendelea kuboresha takwimu za wadeni wa mikopo iliyotolewa toka mwaka 1994. Hadi sasa jumla wadaiwa 113,240 wametambuliwa. Kiasi kinachodaiwa ni **Sh 51,103,685,914** na kiasi kilichokusanywa hadi mwezi Juni, 2007 ni **Sh 53,616,011.22**

- Ilishirikiana na Vyuo vya Elimu ya Juu, Wizara/Idara za Serikali na taasisi zingine kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa mikopo na ukusanyaji wa madeni kutoka kwa waliokopeshwa .
- Ilitoa elimu kwa wadau wa mikopo – wanafunzi na umma kwa ujumla kuhusu dhana ya uchangiaji gharama za elimu na dhana ya mkopo na urejeshwaji wake kwamba dhana hizi hazikinzi bali zinakwenda pamoja.
- Ilikamilisha marekebisho ya Sheria ya Bodi ya Mikopo Na.9 ya mwaka 2004. Sheria iliyorekebishwa itawasilishwa Bungeni mwezi Agosti 2007.
- Ilijiri wafanyakazi 47 ili kuimarisha utendaji wake.

BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI

33. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi lilitokeleza yafuatayo:

- Kukagua na kutoa Usajili kamili (Full Registration) kwa vyuo kumi na nane (18) na usajili wa muda (Provisinal Registration) kwa vyuo tisa (9).
- Kutathmini na kutoa Ithibati kamili (Full Accreditation) kwa vyuo vitano (5) ambavyo ni: (i) National College of Tourism – Dar es Salaam, (ii) Mineral Resources Institute – Dodoma, (iii) Pasiansi Wildlife Training Institute – Mwanza, (iv) College of Business Education (CBE) – Dar es Salaam na (v) CBE – Dodoma. Pia Baraza lilitoa Ithibati ya muda (Provisional Accreditation) kwa vyuo vinane (8) ambavyo ni: (i) Shukran International College (Mbeya), (ii) Tengeru Community Development Training Institute – Arusha, (iii) Newman Institute of Social Work – Kigoma, (iv) Institute of Adult Education – Dar es Salaam, (v) Centre for Educational Development in Health – Arusha, (vi) Institute for Information Technology – Dar es Salaam,

(vii) Institute of Procurement and Supply – Dar es Salaam na (viii) Rungemba Community Training Development Institute – Iringa.

- Kuviwezesha vyuo 31 kuweka mfumo wa kuthibiti na kuhakiki ubora wa elimu na mafunzo yatolewayo na vyuo hivyo.
- Kuidhinisha mitaala inayozingatia umahiri kwa programu ishirini (20) za ngazi ya stashahada.
- Kuratibu uendeshaji wa mitihani ya ufundi katika mfumo mpya wa “National Technical Awards” (NTA) katika vyuo kumi na saba (17).
- Kuhakiki sifa za walimu katika vyuo vya ufundi 55 na kutoa usajili kamili (Full Registration) kwa walimu 431 na usajili wa muda (Provisional Registration) kwa walimu 156.
- Kukamilisha uwekaji wa mfumo wa kumbukumbu kwa njia ya kompyuta (Database) za walimu katika vyuo vya ufundi. Mfumo huo umeanza kutumika kwa kuweka kumbumbu za sifa na taarifa zingine za walimu waliosajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

CHANGAMOTO ZILIZOPO MBELE YETU

34. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio hayo pia zipo changamoto kama zifuatazo:

- Kuongeza udahili hadi kufikia 12.5% ya wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita ili wapate nafasi za kujiunga na vyuo Vikuu ifikapo mwaka 2010.
- Kuhamasisha wanafunzi husasan wanafunzi wa kike ili wapende na kupata nafasi kusomea fani za sayansi na ufundi.
- Kuboresha huduma za mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya juu hususan kutambua wahitaji halisi.

- Kuongeza idadi na ubora wa Taasisi za Elimu ya Juu, ili kuendana na viwango vya ubora vya Kimataifa (Quality Assurance and Relevance).
- Kuwekeza zaidi katika utafiti ili kukidhi mahitaji ya maendeleo nchini.
- Kuandaa wanataaluma wa kutosha wenye sifa zitakazotakiwa katika baadhi ya fani.
- Kuhamasisha jamii iwe na mwamko wa kuchangia kwa hiari maendeleo ya elimu kupitia Mfuko wa Elimu.

MALENGO YA BAJETI YA MWAKA 2007/2008

35. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/08 wizara yangu kupitia Idara na Taasisi zake imejiwekea malengo yafuatayo.

IDARA YA ELIMU YA JUU

36. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Idara ya Elimu ya Juu inatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudhamini wanafunzi 1,772 wa shahada ya kwanza ya udaktari (MD) kati ya hao 50 ni udaktari wa meno (DDS) katika vyuo vikuu vitano vya Sayansi ya Afya nchini. Vyuo hivi ni (i) Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili (ii) Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Hubert Kairuki (iii) Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi za Afya Bugando (iv) "Kilimanjaro Christian Medical College na (v) "International Medical and Technological University".
- Kudhamini wanafunzi tisini (90) raia wa Uganda, katika utaratibu wa kubadilishana wanafunzi wa shahada ya kwanza katika vyuo vikuu vya Afrika Mashariki.

- Kudhamini mafunzo ya wanafunzi watano (5) raia wa China, ikiwa ni kutekeleza mkataba wa ushirikiano kati ya Tanzania na China.
- Kuendelea kuelimisha umma kuwa dhana ya uchangiaji gharama za elimu ya juu na dhana ya mikopo hazikinzi bali zina kwenda pamoja.

Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Elimu ya Juu ya mwaka 1999, na kuisambaza kwa wadau.

- Kuendelea kudhamini mafunzo ya wanataaluma themanini (80) kutoka vyuo vikuu vya umma.

Kuendeleza ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kuhuisha Sheria ya Vyuo Vikuu Na. 7 ya mwaka 2005.

IDARA YA ELIMU YA UFUNDI

37. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Idara ya Elimu ya Ufundi inatarajia kutekeleza yafuatayo:

Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya mwaka 1996 na kuisambaza kwa wadau.

Kudhamini mafunzo kwa wanafunzi 1,800 katika ngazi ya Ufundi Sanifu katika Vyuo na Taasisi za Ufundi zilizo chini ya Wizara.

Kuhuisha Sheria Na. 9 ya mwaka 1997 iliyounda Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Kugharimia mafunzo ya watumishi saba (7), wawili (2) mafunzo ya muda mrefu na watano (5) mafunzo ya muda mfupi.

IDARA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

38. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2007/2008 Idara ya Sayansi na Teknolojia inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

Kuwekeza zaidi katika utafiti pamoja na matumizi ya Sayansi na Teknolojia.

Kukamilisha uandaaji wa Sera ya kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu Tanzania.

Kutoa elimu kwa umma kupitia Redio, luninga, majarida na vipeperushi juu ya umuhimu wa utumiaji wa sayansi na teknolojia katika kukuza uchumi na kuondoa umasikini.

Kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Taasisi ya Kujenga Uwezo wa Maarifa na Kuendeleza Sayansi, Teknolojia na ubunifu Afrika (Nelson Mandela African Institute of Science and Technology- Arusha Campus).

Kutayarisha Sera ya Teknolojia ya Nyuklia nchini.

- Kuanzisha kituo cha kilimo na Bioteknolojia cha Taifa kitakachojengwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. (National Agricultural Biotechnology Centre Affiliated to the Third Component of International Centre of Genetic Engineering and Biotechnology in Cape Town – South Africa). Kituo hiki kitasaidia kukuza uwezo wa wataalam katika masuala ya bioteknolojia na kuwawezesha kuwasialiana Kitaifa na Kimataifa.
- Kuendeleza mkakati wa uhamasishaji wanafunzi na hasa wa kike ili waweze kujiunga na masomo ya sayansi, teknolojia na uhandisi katika ngazi mbali mbali za elimu.
- Kuendeleza majadiliano kati ya Tanzania na India kuhusu ushirikiano katika masuala ya Elimu ya Sayansi, Teknolojia na katika uanzishwaji Vituo vya Sayansi na Teknolojia (Science Parks).

Kuridhia mikataba yote inayosimamiwa na IAEA ili kuwezesha ushirikiano katika upatikanaji wa teknolojia ya nyuklia na usimamizi wa kinga ya mionzi kwa Taasisi mbalimbali hapa nchini.

Kuhuisha Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

IDARA YA SERA NA MIPANGO

39. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Idara ya Sera na Mipango inatarajia kutekeleza yafuatayo:

Kuratibu mpango wa mwaka wa pili wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005-2010.

- Kupitia na kutathmini gharama halisi ya kumwelimisha mwanafunzi Elimu ya Juu (Student Unit Cost).
- Kukamilisha programu maalum ya uendelezaji wa Elimu ya Juu na Ufundi (Quickwin Program) itakayowezesha Benki ya Dunia kusaidia Wizara na Taasisi zake katika maeneo yafuatayo:
 - Kuandaa wataalam wengi na bora katika maeneo muhimu na yenye kipaumbele kwa ajili ya maendeleo ya taifa.
 - Kuandaa walimu bora na wa kutosha hususan katika masomo ya sayansi, hisabati na lugha ili kukidhi mahitaji ya shule za sekondari na vyuo vikuu.
 - Kuimarisha utendaji kazi wa Taasisi za huduma za Elimu ya Juu na Ufundi.
 - Kuimarisha matumizi bora ya TEKNOHAMA katika ufundishaji katika Taasisi za Elimu ya Juu na Ufundi.

- Kuchambua mapendekezo ya mtaalamu mwelekezi kuhusu vyuo 170 ili kuboresha matumizi yake.

Kuratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo 30, kati ya miradi hiyo 18 ni miradi inayofadhiliwa na fedha za ndani na miradi 12 fedha za nje.

- Kukamilisha mpango mkakati wa muda mrefu wa kupanua na kuendeleza Elimu ya Juu (Higher and Technical Education Development Programme).

Kuratibu shughuli za ushirikiano wa Kimataifa.

IDARA YA UTAWALA NA UTUMISHI

40. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Idara ya Utawala na Utumishi inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Kuajiri Watumishi 33 kwa ajili ya Makao Makuu na Chuo cha Ufundi Arusha.
- Kugharamia mafunzo mbalimbali ya Watumishi 67 ya muda mrefu na muda mfupi.
- Kuendelea kutekeleza mkakati wa kuwaelimisha Wananchi na Watumishi kupitia vyombo vya habari kuhusu taratibu za kupata huduma zitolewazo na Wizara.
- Kuendelea kushirikiana na Sekta binafsi katika utoaji wa Huduma zisizo rasmi za Ulinzi, Mapokezi na Usafi Makao Makuu ya Wizara.

Kuendelea kuhamasisha Watumishi kupima afya zao kwa hiari kusan virusi vya UKIMWI na kutoa huduma kwa wale watakojitokeza kuwa wameathirika na VVU/UKIMWI.

Kuhuisha muundo wa Wizara.

VYUO VIKUU

CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM (KAMPASI YA MLIMANI)

41. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2007/2008 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudahili jumla ya wanafunzi 6,500 kati ya hao shahada ya kwanza 4,000 na Shahada ya Uzamili 2,500.
- Kuimarisha Shule ya masomo ya Uzamili (Graduate School) ili kukabiliana na ongezeko la uhitaji wa walimu na watafiti linalotokana na kuongezeka kwa vyuo vikuu vya binafsi na vya umma.
- Kuendelea kuboresha ufundishaji kwa kujenga uwezo wa kutumia teknolojia ya mawasiliano (ICT) katika ufundishaji.

Kuendeleza wafanyakazi kwa kuajiri wanataaluma 215 wa kutoa mafunzo katika ngazi mbalimbali ili kuandaa wataalam wenye elimu bora.

Kuendelea kushirikiana na Serikali pamoja na taasisi za ndani na nje ya nchi kugharamia utafiti kulingana na sera ya utafiti ya chuo na vipaumbele vya taifa letu.

Kuongeza juhudi kuhakikisha matokeo ya utafiti yanasambazwa na kuwafikia walengwa.

Kukamilisha ujenzi wa madarasa mawili yenye uwezo wa kukaliwa na wanafunzi elfu moja (1,000) kila moja. Madarasa hayo yataanza kutumika katika mwaka wa masomo 2007/2008.

Kuendelea na ujenzi wa Makao Makuu mapya ya Taasisi za Sayansi za Bahari eneo la Buyu Zanzibar.

Kukamilisha ujenzi wa jengo litakalotumika kama kituo cha Ujasiriamali.

Kuendelea na awamu ya pili ya Ujenzi wa Mradi wa 'Mlimani City' utakaohusisha ujenzi wa ukumbi wa mkutano, ofisi na nyumba za kuishi.

CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO

42. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kinatarajia kutekeleza yafuatayo:

Kudahili wanafunzi 820 wa shahada ya kwanza na 400 wa shahada za Uzamili.

Kuendelea na miradi ya utafiti wa mbinu bora za kilimo kwa kuhusisha utafiti unaofanyika mashambani mwa wakulima (on-farm and participatory research).

- Kuendeleza warsha/kongamano za kisayansi ambazo wanataaluma na wadau kutoka nje ya nchi watajadili matokeo mbalimbali ya utafiti.
- Kuendelea kutoa elimu na ushauri kwa wakulima.
- Kuendeleza awamu ya kwanza ya ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kukaliwa na wanafunzi 200 kila moja, kati ya mabweni kumi (10) yanayokusudiwa kujengwa.
- Kukarabati majengo ya chuo katika kampasi ya Solomon Mahlangu.

CHUO KIKUU MZUMBE

43. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Chuo Kikuu Mzumbe kinatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudahili wanafunzi 1,730 kati yao 1,300 ni wa shahada ya kwanza na 430 ni wa shahada ya uzamili.

- Kusomesha wahadhiri 15 katika ngazi ya uzamili na wengine 7 katika ngazi ya uzamivu.
- Kujenga mabweni yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 800
- Kukamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300 kampasi ya Mbeya.
- Kukamilisha tafiti 24 za Sayansi ya Jamii.

CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

44. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kinatarajia kufanya yafuatayo:

Kudahili jumla ya wanafunzi 6,698 wa Shahada ya kwanza na Shahada za Uzamili.

- Kutoa mafunzo kwa walimu na wanafunzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania namna ya kufundisha kwa kutumia kompyuta (e-learning).
- Kuendeleza mafunzo ya shahada ya kwanza kwa walimu wa shule za msingi na sekondari.
- Kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike wanaosoma katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kufikia asilimia 35.
- Kuanzisha kitengo cha ushauri (Consultancy Unit) katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Kujenga jengo la mitihani na maabara eneo la Kibaha.

- Kuendelea kutumia teknolojia ya kisasa ya mawasiliano katika vituo vyote vya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na kuimarisha mawasiliano kati ya makao makuu ya Chuo na vituo vya mikoa.
- Kuanza kujenga majengo ya kudumu katika ofisi za mikoa ya Mtwara na Manyara.
- Kununua jengo la RUKWADECO (Rukwa) na PEHCOL (Kilimanjaro) na kulifanyia ukarabati ili litumike kwa shughuli za vituo vya Chuo Kikuu Huria.

CHUO KIKUU CHA DODOMA

45. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Chuo Kikuu cha Dodoma kinatarajia kufanya yafuatayo:

- Kudahili wanafunzi 1,000 wa Shahada ya kwanza katika fani za Elimu, Sayansi ya Jamii na Sayansi za Kompyuta.
- Kuajiri wafanyakazi 214 kati ya hao 80 ni wanataaluma na 134 ni waendeshaji.
- Kuanza ujenzi wa vyuo vitatu ndani ya Chuo (Campus Colleges); Chuo cha Elimu, Chuo cha Sayansi za Jamii na Chuo cha Sayansi za Kompyuta. Ujenzi katika nyuo hivi utahusisha mabweni, bwalo la chakula, vyumba vya mihadhara, madarasa, vyumba vya semina, maabara, ofisi, maktaba, zahanati, barabara na viwanja vya michezo.

CHUO KIKUU CHA TIBA NA SAYANSI ZA AFYA MUHIMBILI

46. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi za Afya Muhimbili kinatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudahili wanafunzi 350 wa shahada ya kwanza na 100 wa shahada za juu.

- Kuendeleza eneo la chuo, Mloganzila Mkoa wa Pwani kwa kujenga barabara kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara (TANROADS).

Kuajiri wahadhiri 200 ili kufikia idadi ya wahadhiri 420.

- Kuweka samani katika mabweni ya wanafunzi yaliyoko barabara ya Chole.
- Kuendelea kufanya tafiti zinazolenga katika kutatua matatizo yanayohusu UKIMWI (chanjo), Kifua Kikuu, Malaria, magonjwa ya kina mama na watoto.

CHUO KIKUU CHA ARDHI

47. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Chuo Kikuu cha Ardhi kinatarajia kutekeleza yafuatayo:

Kudahili wanafunzi 744 wa shahada ya kwanza.

Kutayarisha vyombo mbalimbali vya utawala kwa kuzingatia Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 na Hati Idhini ya Chuo Kikuu cha Ardhi.

- Kurekebisha sera mbalimbali za Chuo ili ziendane na hadhi ya Chuo kikuu kamili.

Kuboresha usimamizi wa idara 22 zitakazoanzishwa rasmi mwaka 2007/08 kwa kuwa na vitivo sita (6) badala ya viwili (2) vilivyopo sasa.

- Kuweka kipaumbele katika utafiti.
- Kuongeza na kuimarisha uhusiano wa kitaalamu na taasisi za kimataifa na kitaifa katika kupanua utafiti na matumizi ya Teknolojia ya mawasiliano.
- Kuimarisha matumizi ya teknolojia ya mawasiliano katika ufundishaji.

- Kuendeleza wanataaluma 47 kati ya hao 27 ngazi ya Udaktari wa Falsafa na 20 ngazi ya Uzamili pamoja na waendeshaji 28.
- Kuendelea na ukarabati wa majengo ya chuo pamoja na miundombinu.
- Kuendelea na ujenzi wa kumbi mbili za mihadhara zinazoweza kukaliwa na wanafunzi 200 kila moja.
- Kuboresha huduma za ushauri nasaha kwa wanafunzi.

VYUO VIKUU VISHIRIKI

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU DAR ES SALAAM

48. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam kinatarajia kutekeleza yafuatayo:

Kudahili wanafunzi 1,500 wa Shahada ya kwanza.

Kuendeleza ujenzi wa madarasa, maabara, ofisi za walimu na upanuzi wa jengo la utawala.

- Kutoa mafunzo maalum kwa wadhiliwa wa kike kwenye fani ya sayansi kwa lengo la kuongeza wahitimu wa kike kwenye fani hiyo.
- Kukamilisha kupanua maktaba na kununua vitabu zaidi vya kufundishia.
- Kununua vifaa vya maabara.
- Kuimarisha miundombinu na matumizi ya teknolojia ya mawasiliano.
- Kushirikiana na Vyuho na Taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hasa kwa shahada ya uzamili na uzamivu

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ELIMU MKWAWA

49. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kinatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudahili wanafunzi 741 wa shahada ya kwanza na 73 wa stashahada.

Kuendeleza juhudi za kujenga ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kukaliwa na wanafunzi 700.

- Kuendelea na ukarabati wa majengo ya chuo kwa ajili ya ofisi, maktaba na zahanati.
- Kuajiri wahadhiri na wafanyakazi waendeshaji kufikia idadi ya wahadhiri 173 na waendeshaji 94. Hivi sasa chuo kina wahadhiri 56 na waendeshaji 65.

CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA USHIRIKA NA STADI ZA BIASHARA MOSHI

50. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Stadi za Biashara Moshi kinatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudahili jumla ya wanafunzi 555 kati ya hao 205 ni kwa ajili Diploma ya Uzamili na 350 ni kwa ajili ya Shahada ya kwanza.
- Kuongeza idadi ya wanafunzi wa kike kufikia 45%.

Kuboresha miundombinu kwa kuimarisha mtandao kwenye maktaba.

- Kuendeleza mafunzo ya wafanyakazi hususan waalimu, kufikia kiwango cha shahada ya Udaktari wa Falsafa.

- Kuboresha utafiti na uchapishaji wa makala mbalimbali kwa lengo la kusambaza elimu ya Ushirika na Biashara.
- Kuimarisha vituo vya chuo katika kanda nne mikoani Mwanza, Iringa, Tanga na Mtwara kwa kuvipatia samani za ofisi vifaa vya kufundishia pamoja na ukarabati wa madarasa.
- Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu Ushirika wa Akiba na Mikopo SACCOS katika maeneo yafuatayo;
 - Wajibu wa wanachama katika SACCOS
 - Wajibu wa wanachama wa vyama vya Ushirika.
 - Utunzaji wa vitabu vya fedha.
 - Uundaji wa SACCOS

TAASISI YA UANDISHI WA HABARI NA MAWASILIANO YA UMMA

51. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Taasisi ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma inatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudahili wanafunzi 100 wa shahada ya kwanza.
- Kuongeza madarasa mawili kwa lengo la kukabiliana na ongezeko la idadi ya wanafunzi.
- Kuanzisha kituo cha televisheni kitakachotumika sambamba na kituo cha redio katika kufundishia.
- Kuanzisha Diploma ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma na Matangazo.

- Kufanya utafiti wa kitaaluma na kitaalam katika nyanja mbalimbali za uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma na Matangazo.

TAASISI YA TEKNOLOJIA DAR ES SALAAM

52. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam inatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudahili wanafunzi 655 wa mwaka wa kwanza.
- Kukamilisha ununuzi na umilikishwaji wa jengo la Shirika la Nyumba la Taifa eneo la Chang'ombe ambalo linatumika kama Bweni la wanafunzi.

Kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la madarasa na maabara.

- Kugharimia mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 21 na ya muda mfupi kwa wafanyakazi 15.
- Kuendesha mafunzo maalum (Pre entry course) kwa wanafunzi wa kike katika kozi za Ufundi/ kwa kushirikiana na Mfuko wa Elimu Tanzania.
- Kuendeleza mapambano dhidi ya maambukizi ya UKIMWI kwa wanajumuiya ya Taasisi.

TAASISI YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA MBEYA

53. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya inatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudahili wanafunzi 175 wa mwaka wa kwanza katika ngazi ya Ufundi Sanifu kati ya hao 20 ni wasichana sawa na 11%.
- Kuendelea kukarabati majengo, mitambo na vifaa mbalimbali vya kufundishia ili viwe katika hali nzuri ya kuendelea kutumika kwa mafunzo.

- Kuanza ujenzi wa Uzio kuzunguka eneo la Taasisi kwa lengo la kuongeza usalama.

Kuendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi 12.

VYUO

CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE

54. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kinatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kudahili wanafunzi 80 wa programu ya Cheti, 320 wa programu za Stashahada na 150 wa programu za Shahada ya Kwanza.
- Kuajiri wanataaluma 20 na wafanyakazi waendeshaji 14 ili kumudu majukumu ya Chuo.
- Kuanza kuendesha programu ya Shahada ya Masuala ya Jinsia katika Maendeleo.
- Kugharamia mafunzo ya wanataaluma 10 na wafanyakazi waendeshaji 5.

CHUO CHA UFUNDI ARUSHA

55. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka 2007/2008 Chuo cha Ufundi Arusha kinatarajia kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kudahili wanafunzi 186 katika ngazi ya Ufundi Sanifu kati yao 33 ni wanafunzi wa kike sawa na 18%.
- Kuanzisha kozi mpya ya elektroniki na mawasiliano.
- Kugharimia mafunzo ya walimu kumi na wawili (12). Kati yao nane (8) Shahada ya Uzamili na wanne (4) katika ngazi ya udaktari wa falsafa.

- Kukarabati hosteli ya wavulana.
- Kukarabati nyumba 7 zilizopo kwa ajili ya walimu na watumishi wengine.

TUME

TUME YA TAIFA YA UNESCO

56. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2007/2008 Tume ya Taifa ya UNESCO inatarajia kufanya yafuatayo:

- Kuliandaa Taifa na ujumbe wake utakaohusisha viongozi wa ngazi za juu Serikalini na wataalamu mbalimbali katika Kikao cha 34 cha Mkutano Mkuu wa UNESCO kitakachofanyika tarehe 16 Oktoba hadi 03 Novemba, 2007 Paris, Ufaransa.
- Kuratibu utekelezaji wa Programu ya kuhifadhi Historia ya Ukombozi Barani Afrika (African Liberation Heritage Programe).
- Kukamilisha taratibu za kuiwezesha Tume ya Taifa ya UNESCO kuwa chombo cha Serikali kinachojitegemea.
- Kuendeleza uimarishaji wa taaluma ya ufundishaji katika elimu ya msingi na sekondari kwa kuimarisha ufundishaji wa walimu chini ya mpango wa UNESCO.
- Kufuatilia uanzishwaji wa UNESCO Chair katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ili kukiwezesha kupata msaada wa kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu katika eneo la Historia (Hitorical Resource Centre).

TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA

57. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Tume ya Vyuo Vikuu inatarajia kutekeleza yafuatayo:

Kutathmini ubora wa programu za masomo za vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki vya hapa nchini kwa lengo la kuziidhinisha;

- Kuelimisha umma kuhusu majukumu ya Tume;

Kutoa machapisho kumi (10) yenye taarifa za kuelimisha umma kuhusu majukumu ya Tume, ufanisi wake, na kutoa miongozo kwa vyuo vikuu nchini kuhusu udhibiti wa ubora wa elimu ya juu;

- Kuendelea kutathmini vyeti vya wahitimu vitakavyowasilishwa katika Tume ili kutambua uhalali wake.
- Kutathmini mipango ya kuanzisha au kuhuisha vyuo vikuu kumi (10) kwa lengo la kutoa hati husika
- Kuendelea kuratibu maonyesho ya Elimu ya Juu.
- Kukamilisha mfumo wa tuzo (National Qualification Framework).

TUME YA TAIFA YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

58. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia inatarajia kutekelza yafuatayo:

- Kuendelea kuratibu na kuendeleza utafiti nchini ikiwa ni pamoja na:
 - Kuratibu tafiti za kisayansi katika maeneo yenye kipaumbele na kuwawezesha wataalamu wa taasisi za Utafiti na Maendeleo kujenga uwezo wao kitaalamu.
 - Kusimamia na kuendeleza shughuli za bioteknolojia nchini.
 - kuhamasisha ushirikiano wa wanasayansi kitaifa, kikanda na kimataifa.
 - Kupanua masjala ya utafiti katika maeneo ya wanataaluma.

Kuendelea kuhawilisha Teknolojia mpya zinazohakikiwa ikiwa ni pamoja na:

- Kuratibu uanzishwaji wa masijala ya teknolojia zilizobuniwa nchini, teknolojia za asilia na zilizohawilishwa kutoka nje.
- Kuwatambua na kuwasaidia wagunduzi na wavumbuzi kwa kushirikiana na Chama cha wagunduzi Tanzania.
- Kuwezesha na kuratibu usimikaji wa mtambo wa kuchoma taka za hospitali katika Hospitali ya Lugalo.
- Kuendeleza Teknolojia ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu huko Morogoro, Dodoma na Dar es Salaam kwa kushirikiana na Serikali za mitaa.
- Kuendelea na uhawilishaji wa Teknolojia ya habari na mawasiliano ikiwa ni pamoja na:
 - Kuimarisha mtandao wa tasisi za Utafiti na Maendeleo.
 - Kuimarisha matumizi ya mifumo ya mawasiliano vijijini.
 - Kuhamasisha wananchi kutumia sayansi na teknolojia katika harakati za maendeleo kupitia vipindi vya redio, luninga na magazeti.
 - Kuandaa kongamano na maonyesho ya Sayansi na Teknolojia ili kuwakutanisha wadau wa Sayansi na teknolojia.
- Kuendeleza nishati ikiwa ni pamoja na:
 - Kukamilisha matayarisho ya juzuu la pili (Volume II) la kitabu cha vyanzo vya nishati Tanzania.
 - Kuhawilisha teknolojia za nishati mbadala za mkaa wa mawe wa kibiolojia (Coal Biomass Briquettes) huko Shinyanga, mkaa utokanao na masalia ya mazao na matumizi ya nishati jua.

TUME YA TAIFA YA NGUVU ZA ATOMIKI TANZANIA

59. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2007/2008 Tume ya Nguvu ya Atomiki Tanzania inatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kuimarisha huduma za matengenezo ya vifaa vya elektroniki, mashine za "X-ray", kinga na upimaji wa mionzi katika vyanzo mbali mbali vya mionzi.

- Kuratibu utekelezaji wa miradi ya kikanda (Afrika) inayogharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki “International Atomic Energy Agency” (IAEA).
- Kuendelea kukusanya mabaki ya vyanzo vya mionzi na kuyahifadhi katika maabara maalumu, iliyoko Makao Makuu ya Tume Arusha.
- Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa ofisi Makao Makuu ya TUME na kuanza awamu ya pili ya ujenzi wa maabara tatu.
- Kuendelea na ukaguzi wa minara 50 ya simu za mikononi.
- Kukamilisha na kuendesha kituo (Radiological Monitoring Station, RMS) cha kudhibiti majaribio ya silaha za nyuklia chini ya mkataba wa Comprehensive Test Ban Treaty of Nuclear Weapons (CTBT) ambayo Tanzania ili uridhia

MAMLAKA YA ELIMU TANZANIA

60. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Mamlaka ya Elimu Tanzania inatarajia kutekeleza yafuatayo:

Kutathmini utendaji wa Mamlaka ya Elimu Tanzania toka ilipoanzishwa mwaka 2002, kwa lengo la kupima mafanikio na matatizo yake.

- Kufanya marekebisho ya Sheria Na. 8 ya mwaka 2001 iliyoanzisha Mfuko wa Elimu.
- Kuendeleza ushirikiano na Mifuko ya Elimu ya Halmashauri za Wilaya.
- Kuendelea kutoa ruzuku na mikopo kwa vyuo na shule kwa ajili ya miradi mbalimbali ya elimu.
- Kukuza ushirikiano na wadau wengine wanaoshughulikia elimu, kwa mfano National Council for Technical Education (NACTE), Tanzania Commission for

Universities (TCU), Tanzania Social Action Fund (TASAF), Association of Local Authorities of Tanzania (ALAT) na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ili kuunganisha nguvu za kuleta maendeleo ya elimu nchini.

- Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa lengo la kuboresha ufanisi.
- Kuendelea kuelimisha umma kupitia majarida, vipindi vya redio na televisheni, tovuti ya Mamlaka na maonyesho ya kitaifa na kimataifa kuhusu umuhimu wa kuendelea kuchangia Mfuko wa Elimu.

Kuanza ujenzi wa ofisi kwa kushirikiana na Tume ya Vyu Vikuu Tanzania.

BARAZA LA TAIFA LA ELIMU YA UFUNDI

61. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2007/2008 Baraza linakusudia kutekeleza yafuatayo:

- Kukagua na kutathmini taasisi/vyuo vya ufundi 20 kwa ajili ya kuvipatia ithibati.
- Kusajili vyuo 20 vyenye uwezo wa kutoa elimu na mafunzo ya ufundi.
- Kuidhinisha mitaala ya programu za mafunzo 25 yenye kuzingatia umahiri na mahitaji ya soko la ajira.
- Kuratibu mitihani ya ufundi ya kitaifa katika mfumo mpya "National Technical Awards" katika vyuo 20.

Kusajili walimu 400 wanaofundisha katika vyuo vya ufundi.

- Kusimamia na kuviwezesha vyuo 30 kuweka mfumo wa kudhibiti na kuhakiki ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa na vyuo hivyo.
- Kuratibu udahili wa wanafunzi katika vyuo vya ufundi 15 vinavyotoa mafunzo ya Shahada/Stashahada ya Juu.

BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU

62. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2007/08 Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inatarajia kutekeleza yafuatayo:

- Kutoa mikopo katika viwango kati ya asilimia 0 na 100 kulingana na uwezo wa kiuchumi wa kila mwombaji katika ada, elimu kwa vitendo na mahitaji maalum ya vitivo.
- Kukamilisha ajira ya wafanyakazi 33 wa uchambuzi na utoaji mikopo ili kuondoa tatizo la watumishi katika eneo hilo.
- Kuongeza kasi ya kukusanya madeni kutoka kwa waliokopa kuanzia mwaka 1994. Bodi ina lengo la kukusanya Sh 1.2 billioni.
- Kuendelea kuelimisha umma kuwa dhana ya uchangiaji gharama za elimu ya juu na dhana ya mikopo hazikinzi bali zinakwenda pamoja.
- Kutoa mikopo kwa wavulana waliohitimu kidato cha 6 na kupata daraja la 2 pamoja na wale watakaochukuwa masomo ya Sayansi.
- Kuendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wa elimu wanaostahili katika maeneo yafuatayo:

Ada ya masomo

Chakula na Malazi

Vitabu na viandikio

Elimu kwa vitendo

Mahitaji maalumu ya vitivo

Utafiti.

- Kuongeza kiwango cha mikopo kwa ajili ya chakula na malazi kutoka Sh 3,500 kwa siku hadi Sh 5,000.

MAAZIMIO NA MWELEKEO WA BAJETI YA MWAKA 2007/08

63. **Mheshimiwa Spika**, kimsingi bajeti hii inazingatia umuhimu wa ukuzaji rasilimali watu kwa ajili ya maendeleo endelevu, kama msingi wa mkakati wa kupiga vita umaskini. Kwa hali hii maeneo ambayo yamepewa kipaumbele katika mwaka wa fedha 2007/2008 ni kama yafuatayo:

Kuongeza idadi ya wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka 68,029 mwaka 2006/2007 hadi 75,346 mwaka 2007/2008 sawa na ushiriki wa 1.43 % ya rika husika.

Kuanzisha mpango wa muda mrefu wa uendelezaji Elimu ya Juu na Ufundi (Higher and Technical Education Development Programme) ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi linalotokana na mafanikio ya Mpango wa Elimu ya Msingi (MEM) na Sekondari (MES).

Kuanzisha mpango maalum wa uendelezaji wa Elimu ya Juu na Ufundi (Quickwin Program) utakaowezesha Benki ya Dunia kusaidia Wizara na Taasisi zake kutoa elimu bora.

- Kuendelea kuelimisha umma kuwa dhana ya uchangiaji gharama za elimu ya juu na dhana ya mikopo hazikiniani bali zinakwenda pamoja.
- Kuendelea kukusanya madeni kwa wale waliokopa kuanzia mwaka 1994/95, ili wanafunzi wengi zaidi waweze kufaidika na Mfuko huu.
- Kukamilisha uhuishaji wa Sera za Elimu ya Juu, Ufundi na Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.
- Kuongeza na kubuni vyanzo vya mapato kwa ajili ya Mfuko wa Elimu ili kuufanya uwe endelevu, ili kukidhi mahitaji ya kuongeza ubora wa Elimu, upatikanaji wake na kwa usawa.

Kuimarisha ukarabati wa Vyuo Vikuu Vishiriki vya Dar es Salaam, Mkwawa pamoja na Vitivo vya Elimu vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa lengo la kukidhi mahitaji ya walimu bora na wa kutosha wa Sekondari.

- Kuendeleza ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma utakaohusisha ujenzi wa vyuo vitatu ndani ya Chuo (Campus Colleges); Chuo cha Elimu, Chuo cha Sayansi za Jamii na Chuo cha Sayansi za Kompyuta. Ujenzi katika nyuo hivi utahusisha mabweni, bwalo la chakula, vyumba vya mihadhara, madarasa, vyumba vya semina, maabara, ofisi, maktaba, zahanati, barabara na viwanja vya michezo.
- Kuendeleza ujenzi wa Taasisi ya Nelson Mandela, katika eneo la kudumu lililoko Karangai katika Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru, Arusha.

- Kuimarisha matumizi ya TEKNOHAMA kwa ajili ya ufundishaji (e-learning), Utawala (e-government), Biashara (e-commerce) na Mawasiliano (communication).
- Kuwekeza zaidi katika utafiti pamoja na matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu na kusambaza matokeo ya tafiti kwa walengwa.
- Kuongeza idadi ya rasilimali watu kwa kuongeza idadi ya wataalam kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi waliofaulu katika daraja la pili wavulana na wanaochukua masomo ya Sayansi. Aidha, Serikali itaongeza kiwango cha mkopo kwa ajili ya malazi na chakula kutoka Sh 3,500 hadi Sh 5,000.

HITIMISHO

64. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wahisani na wadau mbalimbali kwa michango yao mikubwa katika Wizara yangu. Wahisani hao ni pamoja na: Marekani, Sweden, Norway, Uholanzi, Japan, Ubelgiji, Jamhuri ya Korea ya Kusini, China, Cuba, Algeria, Urusi, Poland, Benki ya Dunia na Umoja wa Mataifa. Aidha, Mashirika mengine ni pamoja na UNESCO, Jumuiya ya Madola, International Atomic Energy Agency, Third World Academy of Sciences, International Foundation for Sciences na sida. Naomba waendeleo na moyo huo nasi tunaahidi kuendeleza ushirikiano huu kikamilifu.

65. Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha Wizara yangu kutekeleza mipango iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2007/2008, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinisha jumla ya **Sh. 287,875,797,000**. Kati ya fedha hizo **Sh. 240,443,408,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Sh 47,432,389,000** ni kwa matumizi ya maendeleo.

66. **Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa napenda kukushuru wewe binafsi, Naibu Spika pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba yangu. Aidha, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara **www.msthe.go.tz**.

67. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

KIAMBATISHO NA. 1

FEDHA ZINAZOOMBWA KWA MATUMIZI YA KAWAIDA FUNGU 68 MWAKA 2007/2008

KIFUNGU	IDARA	FEDHA ZILIZOIDHINISHWA MWAKA 2006/2007	FEDHA ZINAZOOMBWA MWAKA 2007/2008
1001	UTAWALA NA UTUMISHI	2,634,943,800	2,146,473,600
1002	UHASIBU	150,452,000	245,678,500
1003	SERA NA MIPANGO	577,165,800	686,359,800
2001	TUME YA UNESCO	322,005,700	381,040,900
3001	ELIMU YA JUU	150,947,659,500	221,249,230,700
3002	ELIMU YA UFUNDI	10,492,655,300	12,200,425,200
3003	SAYANSI NA TEKNOLOJIA	2,485,335,900	3,534,199,300
	JUMLA	167,610,218,000	240,443,408,000

KIAMBATISHO NA. 2

FEDHA ZINAZOOMBWA KWA MATUMIZI YA MAENDELEO FUNGU 68 MWAKA 2007/2008

KIFUNGU	IDARA	FEDHA ZILIZOIDHINISHWA MWAKA 2006/2007		FEDHA ZINAZOOMBWA MWAKA 2007/2008	
		FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE
1001	UTAWALA NA UTUMISHI	-	63,000,000	-	250,000,000
1002	UHASIBU	-	-	-	-
1003	SERA NA MIPANGO	1,300,000,000	3,000,000,000	400,000,000	-
2001	TUME YA UNESCO	-	-	-	-
3001	ELIMU YA JUU	17,425,998,000	13,409,947,000	24,659,000,000	18,435,139,000
3002	ELIMU YA UFUNDI	3,400,000,000	600,000,000	1,700,000,000	388,250,000
3003	SAYANSI NA TEKNOLOJIA	3,050,000,000	-	1,600,000,000	-
	JUMLA	25,175,998,000	17,072,947,000	28,359,000,000	19,073,389,000
	JUMLA KUU	42,248,945,000		47,432,389,000	

KIAMBATISHO NA. 3

MAOMBI YA FEDHA FUNGU 68

KIFUNGU	DARA	FEDHA ZILIZOIDHINISHWA 2006/2007				FEDHA ZINAZOOMBWA 2007/2008			
		FEDHA ZA KAWAIDA	FEDHA ZA MAENDELEO		JUMLA KUU	FEDHA ZA KAWAIDA	FEDHA ZA MAENDELEO		JUMLA KUU
			FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE			FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	
1001	UTAWALA NA UTUMISHI	2,634,943,800	-	63,000,000	2,697,943,800	2,146,473,600	-	250,000,000	2,396,473,600
1002	UHASIBU	150,452,000	-	-	150,452,000	245,678,500	-	-	245,678,500
1003	SERA NA MIPANGO	577,165,800	1,300,000,000	3,000,000,000	4,877,165,800	686,359,800	400,000,000	-	1,086,359,800
2001	TUME YA UNESCO	322,005,700	-	-	322,005,700	381,040,900	-	-	381,040,900
3001	ELIMU YA JUU	150,947,659,500	17,425,998,000	13,409,947,000	181,783,604,500	221,249,230,700	24,659,000,000	18,435,139,000	264,343,369,700
3002	ELIMU YA UFUNDI	10,492,655,300	3,400,000,000	600,000,000	14,492,655,300	12,200,425,200	1,700,000,000	388,250,000	14,288,675,200
3003	SAYANSI NA TEKN.	2,485,335,900	3,050,000,000	-	5,535,335,900	3,534,199,300	1,600,000,000	-	5,134,199,300
JUMLA YA MAOMBI		167,610,218,000	25,175,998,000	17,072,947,000	209,859,163,000	240,443,408,000	28,359,000,000	19,073,389,000	287,875,797,000

KIAMBATISHO NA. 4**TAFITI MBALIMBALI ZILIZOFANYIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2006/2007**

NA	TAASISI	TAFITI
1.	CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM	<ul style="list-style-type: none">• Kuainisha uhusiano wa kimazingira na shughuli za kila siku za binadamu katika maeneo ya nchi yenye ukame hasa Kondoa, Dodoma ili kuongeza uelewa na utunzaji wa mazingira yanayowazunguka wananchi katika maeneo hayo na shughuli zao za kila siku hususan za kilimo na ufugaji.
		<ul style="list-style-type: none">• Kuainisha tafiti na mikakati ya kuendeleza ujasiriamali na biashara ndogo ndogo nchini kwa lengo la kujenga jamii yenye watu wenye uwezo wa kujiajiri na kujitegemea kiuchumi.
		<ul style="list-style-type: none">• Kuainisha uelewa na mwenendo unaosababisha ajali za barabarani jijini Dar es Salaam na mbuga za wanyama Kupunguza matukio na uwingi wa ajali nchini kwa Watumiaji wa barabara.
		<ul style="list-style-type: none">• Utafiti wa upembuzi yakinifu wa miamba yenye madini ya dhahabu ili Kukuza

		sekta ya madini nchini na hivyo kuongeza pato la Taifa.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti wa kutengeneza vifaa vyenye ufanisi zaidi kwa kutengenezea nguvu mbadala za mionzi ya jua na matumizi mengine ya viwandani Kuwapatia wananchi nishati mbadala na hivyo kuboresha maisha yao.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti wa bioteknolojia na juu ya ubadilishaji wa vinasaba katika matumizi mbalimbali kama vile magonjwa mbalimbali, na mazao ya chakula na Kuongeza uelewa wa masuala ya vinasaba kwa jamii yote.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti juu ya uboreshaji wa kilimo cha mwani katika mikoa ya Zanzibar, Tanga na Pwani.
		Utafiti wa namna ya kupunguza athari zitokanazo na matetemeko ya ardhi katika maeneo ya bonde la ufa yanayozunguka milima ya Rungwe.
2.	CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO	<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti wa mtambo wa kuangulia vifaranga unaotumia nishati itikanayo na mabaki ya mazao na samadi.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu mbuzi wa maziwa mchanganyiko wa mbuzi wa asili na mbuzi kutoka nchini Norway ambao wameboresha afya na kipato cha wafugaji wa

		mbuzi hao hasa Vijijini .
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu uzalishaji wa miche bora ya matunda na maua (miembe, michungwa, ndimu, parachichi, shelisheli n.k) ambayo imesambazwa sehemu mbalimbali nchini.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu uboresheshaji wa kilimo cha umwagiliaji na mbinu za uvunaji na uhifadhi wa maji ya mvua katika maeneo yenye uhaba wa mvua kama Mwanga, Same, Hombolo, Dodoma na Mwanza.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti juu ya uzalishaji bora wa mifugo kama kuku wa kienyeji na ufugaji nyuki wilaya ya Mvomero.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti wa uzalishaji wa mbegu bora za mazao zinazohimili magonjwa na ukame.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu programu ya mageuzi ya kilimo na maliasili kwa maisha bora unaofadhiliwa na serikali ya Norway.
3.	CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ARDHI	

	NA USANIFU MAJENGO	<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu ukuaji wa miji na athari zitokanazo na ukuaji huo.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu upatikanaji wa ardhi kama haki ya msingi ya binadamu.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utumiaji juu ya uzalishaji utumiaji wa ardhi kama dhamana katika makazi yasiyopimwa jijini Dar es Salaam.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti juu ya uboreshaji wa tathmini na uainishaji wa majengo kama chanzo cha mapato kwa halimahauri katika miko ya Morogoro na Dar es Salaam.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu ushirikishwaji wa wanawake katika kuhifadhi mazingira na matumizi bora ya ardhi na mipango katika maeneo ya ziwa Viktoria. (Mwanza, Kisumu na Jinja).
4.	TAASISI YA TEKNOLOJIA DAR ES SALAAM	<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti juu ya computa zinazotumia umeme mdogo kwa mijini na vijijini ili kupunguza matumizi ya umeme wa gridi.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu matatizo yanayo kabili sekta ya habari na mawasiliano nchini.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu matatizo ya uchafuzi wa mazingira hasa maji ya ardhini kutokana

		na matumizi ya vyoo vya shimo jijini Dar es Salaam.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu viasili na viatilifu vinavoharibu mzingira katika bonde la ziwa Viktoria.

TAFITI MBALIMBALI ZITAKAZOFANYIKA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2007/2008		
	TAASISI	TAFITI
1.	CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Kufanya tafiti mbalimbali zinazolenga kuainisha uhusiano wa masuala ya kijinsia na ukimwi, mazingira, serikali za mitaa, biashara na ukiukaji wa haki za wanawake.

		<ul style="list-style-type: none"> • Kuboresha kilimo cha ufugaji wa samaki (Fish farming).
		<ul style="list-style-type: none"> • Kuendeleza na kuboresha kilimo cha mwani katika pwani ya Zanzibar na Tanzania Bara.
		Utafiti kuhusu aina ya rasiliamali za baharini, matumizi na namna ya kuzihifadhi.
		<ul style="list-style-type: none"> • Kuangalia uwezekano wa kutumia lugha asilia kwa ajili ya kufundishia na kuelekeza (giving instructions).
		Kufanya utafiti ili kupunguza maambukizi ya ukimwi na kuboresha maisha/afya ya waathirika (ikiwa ni pamoja na yatima).
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu maambukizo ya ukimwi kwa mtoto kupitia kwa mama ili kuona ukubwa wa tatizo ili kuweka mikakati ya kuzuia maambukizi hayo. Walengwa ni akina mama wajawazito ambao wameathirika kwa ugonjwa wa ukimwi na Ufahamu wa tatizo hili utawezesha kuweka mikakati ya kinga.
2.	CHUO KIKUU CHA	<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu Ng'ombe aina ya Mpwapwa Breed hutoa maziwa na

	SOKOINE CHA KILIMO	nyama kwa wingu kuliko ng'ombe wa asili.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu malisho ya chakula bora kwa mifugo, ambapo mbegu zake zitaendelezwa na kuhifadhiwa.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu magonjwa ya mifugo na yanavyoenea nchini na jinsi ya kuyadhibiti.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti juu ya kudhibiti viumbe hai waharibifu wa mazao nchini.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti juu ya uzalishaji wa mbegu mpya ya maharage ya soya Mbarali mkoani Mbeya.
		<ul style="list-style-type: none"> • Utafiti kuhusu mazao na mimea ya misituni ilimwayo na uwezekano wa kulima hapa Tanzania. Pia Kuorodhesha na kutathmini lishe na mbinu za uzalishaji wa mbegu katika mikoa ya kaskazini Kilimanjaro, Arusha na Manyara, Dodoma na Singida.
3.	CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA ARDHI NA USANIFU MAJENGO	Utafiti juu ya migogoro ya miradi ya ujenzi na uhirikishwaji wa wanawake.

		Utafiti juu ya matokeo ya MKURABITA na MKUKUTA kwa wanachi wa kipato cha chini.
--	--	---